



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
MFUKO WA TAIFA WA PEMBEJEZO ZA KILIMO**



DIRA

Kuwa kinara chaguo katika kutoa mikopo ya Pembejeo na zana kwa riba nafuu kwa wakulima wadogo katika kuitikia wito na mahitaji ya maendeleo ya Kilimo Tanzania.

DHIMA

Kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wakulima, wadogo nchini Tanzania ili kuboresha maisha ya kaya pamoja na usalama wa chakula wa Taifa.

MADHUMUNI

Kupanua maeneo ya kilimo na kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo.

WALENGWA.

- Vijana na Wanawake wenyewe umri wa miaka 18 hadi miaka 40 ambao wanaojihusisha na shughuli za kilimo,
- Wakulima binafsi;
- Vikundi vilivyosajiliwa vinavyojihusisha na shughuli za kilimo;
- Kampuni zilizosajiliwa zinazojihusisha na shughuli za kilimo;
- Vyama vya Ushirika (SACCOS na AMCOS) na
- Taasisi za Fedha.

MAENEKO YANAYO GHARAMIWA NA MIKOPO YA MFUKO WA PEMBEJEZO

- Uchimbaji wa visima na mifumo ya umwagiliaji ili kuwezesha kilimo cha umwagiliaji;
- Uongezaji thamani wa mazao ya kilimo na mifugo;
- Uhifadhi wa mazao ya kilimo (maghala);
- Kilimo cha mazao ya muda mfupi (Mbogamboga, Viazi, Matunda, Mahindi Mabichi, n.k.);
- Pembejeo za kilimo (mbolea za viwandani, mbegu bora, viutilifu na sumu za kuulia magugu);
- Gharama za uendeshaji wa shughuli za kilimo;
- Mitambo ya mashambani (matrekta ya mikono na mashine za kilimo);
- Miundo mbinu ya kilimo na mifugo.

DHAMANA ZA MIKOPO

- Kwa wakulima binafsi wenyewe mali zisizohamishika. Mali hizi ni kama vile nyumba, mashamba na viwanja vyenye hati miliki
- Kwa makampuni/ Asasi/ Vikundi /SACCOS/AMCOS zenye mali zisizohamishika. Mali hizi ni kama vile nyumba, mashamba na viwanja vyenye hati miliki
- Kwa Wafanyakazi wenyewe mikataba ya kudumu wanaweza kukopeshwa kwa dhamana ya mshahara
- Kwa Taasisi za Kifedha ambazo hazina hati miliki ni nyaraka zote muhimu za usajili kwa mujibu wa sheria pamoja na kiwango cha chini cha mtaji 'minimum core capital' kama inavyopendekezwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa mawasiliano

Mkurugenzi Mtendaji, Mfuko wa Pembejeo, S.L.P 2382, Dodoma, Simu +255 026 26235166
Nukushi/fax: +255 026 2350268, Baruapepe: info@agitf.g.tz